

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA**

**08 MEI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA – TAREHE 08 MEI, 2024**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**272. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga uzio katika Shule ya Sekondari ya Nyalanja Meatu kurahisisha ulinzi wa mali na Wanafunzi wa Bweni wapatao 600.

**273. MHESHIMIWA JANETH MAURICE MASSABURI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mwendokasi inayotoka Kigogo - Tabata Dampo hadi Segerea.

**274. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani kuhakikisha dawa zinapatikana na kukidhi mahitaji katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Mkoa wa Mara.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**275. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha maslahi ya Watumishi wa Umma nchini.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**276. MHESHIMIWA YAHYA ALLY MHATA  
(NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya Utafiti katika Mji Mdogo wa Mtambaswala ili kubaini ni namna gani unaweza kuchangia uchumi wa nchi.

**WIZARA YA NISHATI:**

**277. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL  
MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme cha Kakozi - Tunduma utaanza.

**WIZARA YA KILIMO:**

**278. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI  
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa wa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imefikia hatua gani kuwapatia Vijana 400 Vifaa vya kutengeneza Vihenge visivyoruhusu hewa kwa mujibu wa Ilani ya CCM ya 2020/25.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **279. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali haioni umefika wakati wa kubadilisha Sheria ya mwendo wa magari kutoka Km. 80 hadi kufikia Km. 100 kwa saa.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **280. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi ya kumaliza kero ya maji katika Jimbo la Hai.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **281. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, nini mkakati wa Serikali katika kupunguza baadhi ya Tozo na kufuta zingine ili kuleta unafuu kwa Wavuvi.

**282. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango mkakati gani juu ya Kiwanda cha Nyama kilichopo Shinyanga ambacho hakifanyi kazi kama ilivyokusudiwa.

**WIZARA YA FEDHA:**

**283. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wafanyabiashara kulipwa madai na riba pindi wanapo cheleweshewa malipo.

**284. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itarejesha asilimia 20 ya Kodi ya Ardhi (*Retention*) kwenye Halmashauri kama ilivyopitishwa katika Sheria ya Fedha 2023/2024.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA  
YA HABARI:**

**285. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,  
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itapeleka huduma ya Mawasiliano  
Kata ya Simbai - Hanang’.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA  
MAKAZI:**

**286. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE  
(KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba  
na Maendeleo ya Makazi:-

Je, kuna mpango gani juu ya eneo lililochukuliwa bila  
fidia na halijaendelezwa Kijiji cha Kasesya mpakani  
mwa Tanzania na Zambia.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
08 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**

